# OFISI YA WAZIRI MKUU TAMISEMI

## HALMASHAURI YA WILAYA YA WANGING'OMBE

**SHULE YA SEKONDARI Dr. DUGANGE**

**NJOMBE**

**S.L.P 980**

**SIMU : 0754 63 09 67/0765 52 23 02**

NDUGU MZAZI /MLEZI WA ……………………………….

S.L.P ……………………………………………………….

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI**

**Dr. DUGANGE 2026/2027 WILAYA YA WANGING'OMBE MKOA WA NJOMBE.**

**<u>UTANGULIZI.</u>**

Ninayo furaha kukutaarifu kuwa,mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule hii mwaka 2026/2027. Shule ya Sekondari **Dr. DUGANGE**, ipo katika kijiji cha ITULAHUMBA kata ya **ITULAHUMBA wilaya ya WANGING'OMBE** mkoa wa NJOMBE. Shule ipo kilometa **06** kutoka barabara kuu ya Njombe - Makambako ambapo kituo cha kushuka ni ITULAHUMBA KIBAONI na nauli ya basi kutoka kibaoni hadi shuleni haizidi Tsh 3,000.
Muhula wa masomo utaanza kulingana na mpango wa wizara.

### SARE ZA SHULE NA MAVAZI YA MWANAFUNZI.

#### <u>A: WAVULANA</u>

i. Mashati mawili (02) meupe ya mikono mirefu.
ii. Suruali mbili,moja rangi ya kijani jeshi na ya pili rangi ya zambarau nyeusi mshono wa kawaida na zisiwe modal wala za kubana na kitambaa kiwe istimu namba moja 1. Suruali zote ziwe na marinda mawili kila upande, mifuko mitatu yaani mbele miwili na nyuma mmoja bila kusahau mshono wa turn-up.
iii. Viatu vyeusi vya kamba visivyo na kisigino kirefu jozi mbili.
iv. Soksi nyeusi jozi mbili au zaidi.

v. Mkanda mweusi wa ngozi.
vi. Sweta moja rangi ya kijivu lenye shingo ya **V**
vii. T-shirt ya kutanguliza ndani iwe nyeupe / sweta ya kabashingo (pull neck) nyeusi.
viii. Suruali ya kazi rangi nyeusi.
ix. T-shirt ya kazi yenye kola isiyo na maandishi rangi ya bluu.
x. Tracksut pair moja rangi ya Dark bluu.
xi. Raba za michezo pair moja,
xii. Bukta rangi ya bluu.
xiii. Jacketi jeusi kwa msimu wa baridi tu lisiwe na kofia wala maandishi
xiv. Tai mbili (rangi za suruali)

## B. <u>WASICHANA</u>

**i.** Blauzi 2 nyeupe za mikono mirefu.
**ii.** Sketi mbili (2) moja ya rangi ya kijani jeshi na ya pili rangi ya zambarau nyeusi, mshono rinda box yenye urefu hadi kisigino. Kitambaa kiwe istimu namba 1.
**iii.** Tai mbili (rangi za sketi)
**iv.** Viatu vya kamba vyeusi jozi mbili vyenye kisigino kifupi (siyo yebo wala bajaji)
**v.** Soksi nyeupe ndefu jozi 2 au zaidi
**vi.** Sweta moja rangi ya kijivu lenye shingo ya V.
**vii.** Nguo za ndani (chupi) zaidi ya 4 na tight angalau 2 au zaidi
**viii.** T-shirt nyeupe au sweta ya kabashingo ( pull neck) nyeupe
**ix.** Leso mbili au zaidi
**x.** Nguo za ndani za kutosha
**xi.** Raba za michezo na socksi.
**xii.** Tracksut rangi ya Dack bluu.
**xiii.** Gauni la kishindia rangi ya kijivu (shamba dress 1) mshono wa solo mikono mirefu na urefu hadi kisigino (kitambaa istimu namba 1)
**xiv.** Tshirt yenye kola rangi ya bluu isiyo na maandishi.
**xv.** Jacketi jeusi lisilokuwa na kofia na maandishi au picha kwa msimu wa baridi tu

**ZINGATIO:** Rangi ya hijabu kwa wale wa dini ya kiisilam ziwe nyeupe darasani na nyeusi

Wakati wa kazi.

**MAHITAJI MENGINE YA MUHIMU AMBAYO MWANAFUNZI ANAPASWA KUJA NAYO NI :-**

I) Madaftari counter 10 quire3/4
II) Ream A4 bunda 2
III) Vitabu vya masomo kulingana na tahasusi utakayosoma
IV) Godoro la Dodoma 2.5 x 6 ‘’
V) Mashuka mawili ya rangi ya bluu bahari.
VI) Blanketi zito 1
VII) Vyombo vya chakula (kontena na kijijko)
VIII) Scientific calculator
IX) Tranka au sanduku la kuhifadhia vifaa vyake.

**MICHANGO YA MINGIN**

| S/N | AINA YA MCHANGO | KIASI |
|---|---|---|
| 1 | MCHANGO WA UENDESHAJI WA SHULE | **70,000/=** |
| 2 | TAHADHARI (haitarejeshwa) | **5,000/=** |
| **4** | **KITAMBULISHO CHA SHULE** | **5,000/=** |
| | **JUMLA** | **80,000/=** |

***<u>FEDHA ZOTE ZIWEKWE KWENYE AKAUNTI NO.63210004335 </u>NMB,YENYE JINA LA<u> SHULE YA SEKONDARI Dr.DUGANGE</u>***

i. Jembe moja lenye mpini kwa wanafunzi wote.
ii. Mfagio wa chelelewa na hard bloom moja kwa wanafunzi wa kiume na chelewa na soft bloom moja kwa wanafunzi wa kike.
iii. Ndoo moja ya lita 20 kwa matumizi ya shule na moja ya lita 10 kwa matumizi binafsi
iv. Mafuta ya kujipaka pamoja na kitana
v. Mswaki na dawa ya meno
vi. Kiwi na brash yake

**NB: SIMU, LAINI ZA SIMU NA VYOTE VINAVYOENDANA NA SIMU AU RADIO HAVIRUHUSIWI SHULENI**

## SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE.

Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na.25. ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na.10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya Elimu,sayansi na teknolojia yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Rais TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo yafuatayo;

1. Kusimama na kusalimia mtu yeyote anayemzidi umri wakati wote
2. Fanya usafi wa maeneo uliopangiwa kabla kipindi kinachofuata kuanza.
3. Hudhuria vipindi vyote vya shule kwa kuzingatia ratiba iliyopangwa.
4. Kuwa msafi kwa mawazo,maneno,matendo, nguo na mwili muda wote.
5. Ukiwa na tatizo muone mwalimu mlezi uliye karibu nawe ili akusaidie vizuri na kwa haraka.
6. Uwapo shuleni huruhusiwi kubadili jina.
7. Huruhusiwi kubadili dini uwapo shuleni hadi idhini itolewe na mzazi wako.
8. Tabia ya kutoroka vipindi haitavumilika,ukibainika utachukuliwa hatua za kinidhamu.
9. Utatakiwa kuwa katika sare kamili uwapo shuleni na unaposafiri wakati wa likizo.
10. Kutii kengele na kuwahi kufika mahali unapotakiwa.
11. Ugomvi,matusi,na unyanyasaji wa aina yoyote hauruhusiwi kabisa.
12. Huruhusiwi kuja na vazi la aina yoyote ambalo halihusiani na sare ya shule.

13. Simu ni marufuku kwa mwanafunzi shuleni, ukuonekana nayo utanyang'anywa na utaivunja mwenyewe mbele ya wanafunzi na adhabu nyingine zitaafuata.
14. Shule itatoa namba ya simu ya shule kwa mawasiliano maalumu tu.
15. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali mfano visu.

**Makosa yanayoweza kusababisha kufukuzwa shule mara moja ukibainika nayo ni haya:-**

1. Wizi
2. Uasherati, Ubakaji, na Ushoga.
3. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya.
4. Uvutaji bangi.
5. Makosa ya jinai.
6. Kupigana au kupiga.
7. Kudharau bendera ya Taifa.
8. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
9. Kuoa au kuolewa.
10. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule.
11. Kutoa au kusaidia kutoa mimba.
12. Kugoma,kuchochea, au kuongoza kuvuruga amani na usalama wa watu.
13. Kukataa adhabu kwa makusudi.
14. Kutoroka shuleni.

KARIBU SANA Dr. DUGANGE SEKONDARI

___________

Lize Petro Mulungu
Mkuu wa shule.

MOTTO: "WE ALL NEED BETTER EDUCATION FOR BETTER LIFE"

MAWASILIANO:

MKUU WA SHULE: SIMU 0754 63 09 67 AU 0765 52 23 02

MAKAMU MKUU WA SHULE: 0752 51 93 73
MTAALUMA: 0753 55 04 21

# FOMU MBALI MBALI

- **MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI.**

  **(JAZA KWA HERUFI KUBWA TU)**

**1**.Jina la mwanafunzi (majina matatu)……………………………………………………….

Tarehe ya kuzaliwa ………………… umri…….. Mahali alipozaliwa kijiji ………………………

Wilaya …………………………………Mkoa ……………………………………………

Dini yako ……………………………….Dhehebu……………………………………………

Shule uliyotoka…………………………………………………………………………

**2.** Jina la Baba …………………………………………..Yu hai / alifariki……………..

Jina la Mama ……………………………………………Yu hai /alifariki………………

Jina la mlezi kama baba alifariki…………………………………………………………...

Anwani ya Baba mzazi /mama /Mlezi……………………………………………………..

Kazi afanyayo Baba mzazi/mama /Mlezi ……………………………………………………

(futa lisilohusika)

Jina la mwajiri kama ameajiriwa…………………………………………………………….

Dini ……………………………Dhehebu…………………………………………………

Tahasusi yako………………………. Fani unayopendelea……………………………………

Namba ya simu ya 1.Baba Mzazi/Mama /Mlezi …………………

2.mtu wa karibu…………… uhusiano3…………………….uhusiano………..

| Picha ya mwanafunzi | Picha ya mzazi | Picha ya mama | Mlezi/ ndugu wa karibu. |
|---|---|---|---|
| | | | |

- **FOMU YA VIPIMO VYA AFYA – IJAZWE NA DAKTARI**

**Dr. DUGANGE SS**

**P.O.BOX 980**

NJOMBE

13/05/2026

PART A

The Medical officer

___________________District / Regional / Referral Hospital

P.O.BOX _________

__________________

**THE REQUEST OF MEDICAL EXAMINATION**

Please examine __________________________________________(name of a student) as to his/ her physical and mental fitness for a full time student in this school. The examination should include the following categories of which will render the applicant's ineligibility in case of any defect.

a) Eye-sight ……………………………………………………………………………………………………………

(b) Hearing……………………………………………………………………………………………………………

(c) Limbs……………………………………………………………………………………………………………

(d) Speech…………………………………………………………………………………………………………

(e) Leprosy…………………………………………………………………………………………………………

(f) Epilepsy……………………………………………………………………………………………………………

**g) Neuroses ……………………………………………………………………………………………………………**

h) Other serious Diseases…………………………………………………………………………………………….

i) Pregnancy for girls only ……………………………………………………………

**PART B: MEDICAL CERTIFICATE:**

(To be completed by a government medical officer)

I have examined the fitness of the above candidate and consider that he/she is physically fit/unfit and mentally fit/unfit for a full time schooling course for further studies.

Name ………………………………………………… Signature and office stamp…………………..

Station……………………………………………… Designation………………………………… Date ………………………